AGOSTI 2022

Dart Jarida

Toleo la Mtandaoni.

# Mtoa Huduma Mpya wa Mabasi katika Mradi wa DART apatikana.



*Mtendaji Mkuu DART, Dr. Edwin P. Mhede akikagua mkataba wa makubaliano ya kazi (Internal Audit Charter) baina ya DART na kamati mpya ya ukaguzi kabla ya kuzisaini, Agosti 1, 2022 Ubungo Maji, Dar es Salaam.*

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umekamilisha taratibu za kumpata mtoa huduma mpya ya Mabasi katika Mradi wa DART Awamu ya Kwanza, uamuzi ambao utaimarisha na kuboresha huduma ya usafiri Dar es salaam.

Kwa mujibu wa taarifa ya DART iliyowasilishwa katika kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya umma (PIC) Agosti 29, 2022 Mtoa huduma huyo wa Mabasi Yaendayo Haraka ni kampuni ya Emirates kutoka Umoja wa Nchi za Kiarabu (UAE).

Hatua hiyo ni miongoni mwa mikakati mahsusi ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mh.Samia Suluhu Hassan ya kuwaondolea kero ya usafiri wakazi wa Dar es Salaam ambapo mradi wa DART ulianzishwa ili kukabiliana nayo.

Kusainiwa kwa mkataba baina ya DART na Mtoa Huduma huyo mwezi Septemba, 2022 kutamwezesha mtoa huduma h-uyo kuongeza idadi ya Mabasi katika Mradi tofauti na iliyokuwepo hivi sasa kupitia Mtoa huduma ya mpito, Kampuni ya UDART.

Naye, Mwenyekiti wa PIC, Mhe. Jerry Silaa akizungumza mara baada ya kupokea taarifa hiyo jijini Dodoma alisema, hatua za kuongeza mshindani wa kutoa huduma ya Mabasi katika mfumo wa DART itaongeza wigo wa ushindani ambao utapelekea kutolewa kwa huduma bora kwa wananchi.

Aidha, katika kuendelea kuboresha huduma zake, Wakala wa DART umeendelea kukamilisha mfumo wa Serikali wa Kielekroniki katika Ukusanyaji Nauli (AFCS) hususani upande wa matumizi ya kadi ambapo mfumo huo unategemewa kudhibiti upoetevu wa mapato.

Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam unatekelezwa katika Awamu sita ambapo awamu ya kwanza imekamilika na huduma inatolewa katika njia kuu inayoanzia Kimara hadi Kivukoni, na tawi la Fire hadi Gerezani pamoja na tawi la Magomeni hadi Morocco. Aidha, Awamu ya Kwanza inahusisha pia huduma katika Njia Mlishi ya Gerezani Muhimbili, Kimara Mbezi, Kimara Mloganzila , Kimara hadi Kituo Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli. Njia Mlishi nyingine ni Kimara hadi Kibaha Pamoja na Shekilango hadi Mwenge.

# DART yahamasisha SENSA

Katika kuhakikisha zoezi la Kitaifa la Sensa ya Watu na Makazi linafanikiwa, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ulijitokeza kuhamasisha Watanzania kushiriki katika zoezi la kitaifa la Sensa ya Watu na makazi iliyofanyika tarehe 23 Agosti 2022




Wakala ulishiriki katika uhamasishaji kwa kutumia tangazo la sauti lililorushwa ndani ya Mabasi 150 yanayotoa huduma maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Tangazo hilo lililotolewa kwa ushirikiano na Mkuu wa Wilaya ya Kibaha Mhe. Sarah Msafiri, lilihamasisha watumiaji wa Mabasi Yaendayo Haraka washiriki kuhesabiwa kwa maendeleo ya taifa.

Aidha, Wakala pia uliandaa jumbe za uhamasishaji katika kurasa za mitandao ya kijamii ya Facebook, Instagram, Twitter Pamoja na Youtube.

# DART yaendeleza Kampeni ya Usalama katika Mfumo wake.

Wakala wa mabasi yaendayo Haraka (DART) umeendeleza jitihata za kufanya kampeni ya usalama katika Mfumo wake ili kupunguza ajali za mara kwa mara hususani katika makutano ya barabara pamoja na maeneo yenye vivuko vya waenda kwa miguu.

Jitihada hizo zinazofanyika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kikosi cha usalama barabarani Makao makuu, inalenga kutoa elimu ya matumizi sahihi ya miundombinu ya DART pamoja na alama za barabarani hususani zile zilizoko katika barabaraba za mabasi yaendayo haraka.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mwezi Agosti 2022 wakati wa kampeni hiyo baadhi ya wadereva wa pikipiki walioshiriki katika zoezi hilo eneo la Shekilango, wamepongeza hatua za Wakala wa DART kupita na kutoa Elimu mara kwa mara kwani inasaidia kupunguza ajali, lakini pia inawakumbusha wanaoendesha vyombo vya moto na baridi wajibu wao wanapokua barabarani.

“Tumekuwa tukishuhudia ajali nyingi sana hapa Shekilango hasa zinazohusisha sisi waendesha pikipiki na Mabasi Yaendayo Haraka. Elimu hii tunayopewa itasaidia kupunguza ajali katika eneo hili” Alisema Innocent Stephano Katibu wa Bodaboda Shekilango. Katibu huyo bodaboda alisema eneo hilo limekua hatarishi kwao hadi kupachikwa jina la machinjioni kutokana na kutokea kwa ajali za mara kwa mara ambazo kwa kiasi kikubwa zimewahusiaha waendesha bodaboda.

Aidha kwa upande wake Katibu wa bodaboda kituo cha Magomeni Bw. Seif Said, alisema eneo la Magomeni Kagera na lenyewe ni hatarishi kwa waendesha bodaboda kwani wengi wao wamekua wakigongwa na Mabasi Yaendayo Haraka kwa kutozingatia sheria za usalama barabarani zinazowataka kukokota vyombo vyao wanapokatiza barabara za Mabasi Yaendayo Haraka kupitia vivuko vya waenda kwa miguu.


Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, kitengo cha usalama barabarani, Dumu Mwalugenge akitoa mafunzo kwa madereva pikipiki (bodaboda na bajaji), eneo la Kibo kuhusu uzingatiaji wa alama usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kutoingilia barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka, wakati wa kampeni ya Usalama katika mfumo wa DART.

“Wiki moja iliyopita tulishuhudia mwenzetu mmoja akipoteza maisha katika ajali kwenye barabara za Mwendokasi, baada ya kufuatilia tuligundua yeye anatokea Kigamboni hivyo hana elimu sahihi ya matumizi ya barabara hasa huku ambako kuna njia ya Mabasi Yaendayo Haraka” Alisema.

Akieleza umuhimu wa kampeni hiyo kwa madereva bodaboda na bajaji eneo la Kimara Korogwe, Afisa Ustawi wa Jamii Mkuu wa DART Bi Anna Gelle, alisema mwendelezo wa zoezi la kutoa elimu kuhusu usalama katika mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka kumesaidia kupunguza idadi ya ajali ambazo zimeendelea kuitia doa taswira nzuri ya mradi huo.

“Lengo la mradi ni kusaidia kupunguza kero ya usafiri wa umma katika Dar es Salaam hivyo kunapokuwa na ajali za mara kwa mara wananchi, kunapunguza imani kwa mradi na kuuona kwamba sio msaada bali ni chanzo cha ajali. DART tuko hapa kuendelea kuwakumbusha wajibu wenu ili muwe salama na mradi pia uendelee kuwa na manufaa kwa wananchi wa Dar es Salaam” Alisema Bi Anna Gelle.

## Mkurugenzi Utawala ataka weledi katika kuhudumia Wateja.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) katika kuboresha huduma zake umefungua Kituo cha Huduma kwa Wateja, ili kupokea na kushughulika malalamiko, na hoja mbalimbali zinazotokea katika Mabasi Yaendayo Haraka.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo kwa maafisa watakaohudumu katika kituo hicho, Mkurugenzi wa Utawala Rasilimali Watu na Mawasiliano wa Wakala Dkt. Eliphas Mollel aliwasisitiza kutoa huduma kwa kuzingatia weledi wakati wanahudumia wateja.

“Abiria ni wateja wetu wakuu na ndio wanaoiwezesha DART kuwepo, wasipokuwepo hao na taasisi yetu haitakuwepo, hivyo ni lazima tuwe wanyenyekevu kwao kwani wao ndio wanaotuweka mjini” alisema Dkt. Mollel.

Aidha, alisema ni muhimu kuwaona wateja kama wafalme na wasichoke kuwahudumia pale wanapowauliza maswali ya mara kwa mara na hata kama wakiuliza maswali ya kuudhi wawapatie majibu kwa upole na kuzingatia maadili katika utumishi.

“Wakala unafanya biashara hivyo ili uweze kupata wateja wengi zaidi ni lazima tuboreshe huduma, kwa maana hiyo uwepo wenu na kituo cha kuhudumia wateja ni dhahiri kwamba wateja wataongezeka hivyo tujitume na tuendelee kuboresha zaidi ” alisema Dkt. Mollel.



Mkurugenzi huyo pia, aliwataka Maafisa hao kuwa maridadi kimavazi na matendo na kuwa tayari kujifunza na kupokea hoja mbalimbali kutoka kwa wateja wa ndani na wa nje yote ikiwa ni katika kuboresha huduma.

Kituo cha Huduma kwa Wateja kilichofunguliwa, kitawawezesha abiria wa Mabasi Yaendayo Haraka pamoja na wateja wengine kupiga simu bila malipo katika namba 0800110147 pale wanapokuwa na maoni, ushauri au msaada kuhusu huduma zinazotolewa.

> *Abiria ni wateja wetu wakuu na ndio wanaoiwezesha DART kuwepo, wasipokuwepo hao na taasisi yetu haitakuwepo, hivyo ni lazima tuwe wanyenyekevu kwao kwani wao ndio wanaotuweka mjini.*

# Kamati mpya ya Ukaguzi yaaswa kuzingatia Weledi.



*Mtendaji Mkuu wa DART, Dr. Edwin P. Mhede (kushoto) akimsikiliza Dr. Augustino Fungo ambaye ni mmoja wa wajumbe wa kamati mpya ya ukaguzi katika hafla ya kuzindua kamati hiyo inayoundwa kwa mujibu wa kanuni za fedha za umma, za mwaka 2001. Wa pili kutoka kushoto ni mwenyekiti wa kamati hiyo, CPA Jamhuri Ngelime akifuatiwa na Meneja Ukaguzi wa Ndani wa DART, CPA Flora Fifi.*

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dr. Edwin P. Mhede ameitaka Kamati Mpya ya Ukaguzi kuzingatia weledi katika kutekeleza majukuu yake ili kuusaidia wakala kutimiza malengo yake yaliyoainishwa wakati wa kuanzishwa kwake.

Alisema hayo Agosti 01, 2022 katika Ofisi za Wakala zilizoko Ubungo Maji Dar es salaam wakati wa uzinduzi wa kamati hiyo iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuzi za Fedha za Umma za mwaka 2001.

Dr.Mhede alisisitiza kuwa mbali na kujikita katika misingi , kanuni , taratibu na sheria za ukaguzi wajiongeze katika kuzingatia misingi ya kibiashara kwani DART inafanya biashara.

"Katika kutekeleza majukumu yenu hakikisheni mnatusaidia katika masuala mazima ya fedha huku mkizingatia kwamba DART inatoa huduma bora na ya kimataifa kwa wakazi wa Dar es Salaam" Alisema Dr.Mhede.

Aidha, Dr. Mhede alitanabaisha kwamba ni vyema kamati pia ikaja na mikakati ya kuuwezesha wakala kujitegemea kimapato badala ya kutegeea ruzuku kutoka serikalini.

Dr.Mhede alisema sheria iliyoanzisha Wakala za serikali katika Ibara yake ya 12 imeelekeza wakala zote kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya kibiashara ili ziweze kujitengenezea vyanzo vyake vya mapato kwa kutumia ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa kamati hiyo CPA Jamhuri Ngelime, alimhakikishia Dr.Mhede kuwa kmati yake itaendelea kufanya kazi kwa viwango ili kuuwezesha mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka kung'ara zaidi.

Kamati ya ukaguzi inajumuisha wajume watano kutoka nje ya wakala ambao ni CPA, Jamhuri Ngelime kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Dr. Augustino Fungo kutoka Taasisi ya Fedha ya (IFM), na Bw. Charles Palapala kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Wengine ni Bw. Moses Abdul kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Serikali pamoja na Mhandisi Yona Malolo kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

*Kamati ya Ukaguzi inaundwa kwa mujibu wa kanuni za fedha za umma za mwaka 2001.*

---

*Kamati hizi zinadumu kwa muda wa miaka mitatu kabla ya kuteuliwa tena.*

# Habari katika picha



Mtendaji Mkuu DART, Dr. Edwin P. Mhede na Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi CPA. Jamuhuri Ngelime wakionyesha mkataba wa Makubaliano ya kazi mara baada ya kusaini katika haflaya kuikaribisha kamati mpya ya Ukaguzi inayoundwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001.



Menejimenti ya Wakala wa DART ikiongozwa na Dr. Edwin P. Mhede (aliyekaa katikati) wakiwa katika picha ya pamoja na Kamati ya Ukaguzi wakati wa hafla ya kuikaribisha kamati hiyo inayoundwa mujibu wa Kanuzi za Fedha za Umma za Mwaka 2001.




Afisa Ustawi wa Jamii Mkuu Bibi. Anna Gelle (katikati) akikagua taarifa za abiria wenye uhitaji waliohudumiwa katika Kituo Kikuu cha Ubungo kutoka kwa Wasaidizi wa Abiria hao ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake kama alivyonaswa na kamera ya DARTJarida Agosti 17, 2022.



Wadau wa Mradi wa DART wakitoa mapendekezo ya maendelezo yapi yafanyike kandokando ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka wakati wa kikao kazi cha mradi wa Maendelezo yatokanayo na Uboreshaji wa usafiri wa Umma (Transit Oriented Development) unaodhaminiwa na Shirika la Maendeleo ya Japan (JICA).

# Habari katika picha



Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Usafirishaji DART, Mhandisi Fanuel Kalugendo (kushoto) akitoa ufafanuzi kwa Maafisa wa Benki ya Dunia wakati walipotembelea Karakana ya Mbagala kuangalia namna karakana za Mradi wa DART zinavyoweza kuboreshwa ili ziweze kuwa na miundombinu ya nishati mbadala za Gesi Asilia na Umeme.



Mtendaji Mkuu wa DART, Dr. Edwin Mhede akikabidhi zawadi kwa Profesa Ayumi Arai kutoka Chuo Kikuu cha Tokyo mara baada ya kumaliza ziara ya kikazi katika Ofisi ya DART iliyolenga kuwajengea uwezo watumishi wa Wakala katika kuboresha huduma zao kupitita taarifa za simu za kiganjani.



Mtendaji Mkuu wa DART, Dr. Edwin P. Mhede akibadilishana mawazo na Maafisa wa Benki ya Duunia na Profesa Ayumi Arai wakati wa hafla ya chakula cha mchana alichowaandalia mara baada ya kumaliza ziara zao za kikazi katika Ofisi na Mfumo wa DART Agosti 09, 2022.



Maafisa TEHAMA wakiongonzwa na Meneja wao, Bw. Ng'wanashigi Gagaga wakiwa katika picha ya pamoja na Wataalam Washauri wa Mfumo wa ukusanyaji nauli wa AFCS kutoka Kampuni ya GSD Plus SAS ya nchini Colombia na Prof. Ayumi Arai kutoka Chuo Kikuu cha Tokyo katika ya hafla ya kuwaaga.

# Habari katika picha



Kaimu Meneja wa Mipango na Usafirishaji, Mhandisi Mohamed Kuganda akiwasilisha mada Mfumo wa DART wakati wa mafunzo ya ndani kwa Maafisa wa Kituo cha Huduma kwa wateja cha DART ili kuwajengea uwezo katika utekutekelezaji wa majukumu yao.



Madereva pikipiki maarufu bodaboda wakikokota vyombo vyao wakati wakikatiza barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka kupitia kivuko cha waenda kwa miguuu, Madereva wengi wa pikipiki wamekuwa wakisababisha ajali kutokana na kukatiza barabara za DART huku wakiendesha vyombo vyao.



Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, kitengo cha usalama barabarani, Dumu Mwalugenge akitoa mafunzo kwa madereva pikipiki (bodaboda na bajaji), eneo la Kibo kuhusu uzingatiaji wa alama usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kutoingilia barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka, wakati wa kampeni ya Usalama katika mfumo wa DART.




Mmoja wa dereva wa pikipiki maarufu kama bodaboda wa eneo la Shekilango, akiuliza swali kwa Afisa Ustawi wa Jamii Mkuu wa DART, Bi. Anna Gelle wakati wakipatiwa mafunzo ya usalama barabarani, Agosti 2022, kwenye kampeni ya Usalama katika mfumo wa DART iliyoendeshwa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.